# Mchomozo wa Usitiari katika Lakabu za Watu Mashuhuri na Maarufu nchini Tanzania

*Hadija Jilala*
*Chuo Kikuu Huria cha Tanzania*

**Ikisiri**

**Makala haya yanachunguza mchomozo wa usitiari katika lakabu za watu mashuhuri na maarufu nchini Tanzania. Lakabu ni majina ya kupanga ambayo baadhi ya watu hupewa au hujipa kutokyana na sifa zao za kimwili, kinasaba, kitabia au kimatendo (Mulokozi, 2019). Majina haya ni maneno au mafungu ya maneno yenye maana iliyofumbatwa. Mara nyingi maneno au mafungu ya maneno hayo huwa na mchomozo wa usitiari ndani yake. Data ya makala haya kwa kiasi kikubwa imekusanywa maktabani kwa mbinu ya usomaji makini na kwa kiasi fulani uwandani kwa kuwasaili wanajamii kuhusu mchomozo wa usitiari katika lakabu hizo. Uchambuzi na uchanganuzi wa data umeongozwa na nadharia ya Jumuishi ya (Giles, 1979) na Nadharia ya Semiotiki (Saussure, 1976). Matokeo ya yanaonesha kuwa lakabu za watu mashuhuri na maarufu ni za kisitiari na zinabeba maana na ujumbe kuhusu ukweli ndani ya jamii husika. Hivyo, mchomozo wa usitiari unaojitokeza katika lakabu hizo unaibua dhamira za kisiasa, kijamii, kimajigambo na kiutamaduni. Kwa ujumla, uchunguzi wa makala unadhihirisha kuwa maumbile ya kimwili, nasaba na tabia au matendo ya mhusika vina nafasi kubwa katika utoaji wa lakabu za watu mashuhuri na maarufu katika jamii ya Watanzania.**

**Maneno Muhimu:** *Mchomozo, Lakabu, Usitiari, Majina, Ishara*

## Utangulizi

Makala hii inalenga kuchunguza mchomozo wa usitiari katika lakabu zinazoibuka na kupewa watu mashuhuri wa kitaifa na watu maarufu nchini Tanzania. Watu mashuhuri au watu muhimu ni watu ambao hupewa upendeleo maalumu katika upataji wa huduma kutokana na hadhi zao za juu katika jamii, mfano viongozi wakuu wa nchi. Kwa upande mwingine, watu maarufu ni wale ambao wanahusishwa na bidhaa, chapa au burudani fulani, mfano, wafanyabiashara, wasanii, wanamichezo na wengineo. Katika jamii nyingi za Kiafrika, utoaji wa lakabu haufanyiki kiholela bali huzingatia vigezo, taratibu na kanuni fulani zinazobeba maudhui au maana ya jina hilo kulingana na mila na desturi za jamii husika (Muzale, 1998). Kwa kawaida, kila kiumbe hupewa jina na binadamu ili kusaidia utambuzi wa haraka wa kinachorejelewa. Katika imani nyingi za Kiafrika na duniani kwa ujumla, majina ya viumbe ni muhimu sana. Kwa sababu jina la mtu huwa ni zaidi ya neno linalomtambulisha mtu mmoja na mwingine katika jamii husika.

Katika maisha ya kila siku, utamaduni huambatana na mazingira na muktadha wa jamii husika. Miongoni mwa mambo ambayo yanafungamana na utamaduni ni mchakato wa utoaji wa majina kama utambulisho wa mtu, kitu ama mahali ndani ya jamii. Kwa mfano, Mutembei (2009:31) anaeleza kuwa baadhi ya majina yanatambulisha mtu eneo analotoka, tabia na sifa yake. Majina yana umuhimu mkubwa kwa wote, watu wanaopewa majina hayo, pia kwa jamii inayotoa majina hayo. Mtu anayepewa jina huwa amepewa utambulisho na kuwa sehemu ya jamii husika. Kupitia jina, mtu huwa ni sehemu ya historia ya jamii, pia majina hutofautisha matendo ya mtu mmoja na mwingine. Uhusiano wa jina na utambulisho ni aina ya alama ya mahusiano kati ya mtu na jamii husika. Kwa kumpa mtu jina, jamii inatambua uwepo wa mtu huyo na majukumu yake katika jamii.

Tukimrejelea Funk (1997) yeye anaeleza kuwa mchakato wa utoaji jina hueleza mengi kuhusu mwanadamu na jinsi anavyohusiana na ulimwengu unaomzunguka. Anaendelea kusema kuwa, utoaji

jina ni tendo kama matendo mengine yoyote, na limo katika muktadha wa kisiasa. Hivyo, kuita mtu au kitu jina fulani ni tukio la kisiasa. Vilevile kutoa jina kunaibua masuala ya mtu mmojammoja na masuala ya kijamii. Kwa kuibua masuala ya kijamii, ni wazi kwamba majina huweza kuibainisha jamii moja na kuipambanua au kuitofautisha na jamii nyingine. Kwa upande wake Muzale (1998) anafafanua kwamba, kutoa jina ni kutoa maana. Majina ya binadamu yanaweza kutusaidia kuwa na mkabala mwingine katika Isimujamii na Isimuhistoria wa kujifunza vipengele vya kihistoria na kijamii katika jamii husika. Maelezo haya yanabainisha wazi kwamba, majina ni kipengele muhimu katika kuelezea masuala yanayohusu jamii na historia yake, hivyo, kuwa sehemu ya utambulisho wa jamii hiyo.

Hivyo basi, katika jamii nyingi za Kiafrika, majina yana athari katika tabia ya mtoto, mafanikio ya mtoto na hata maendeleo ya mtoto ya baadaye. Kwa sababu jina humtambulisha mtu eneo analotoka, huashiria tabia yake, sifa zake, imani na fikra zake. Aidha, lakabu nazo hujenga athari fulani kwa jamii na kwa mhusika aliyepewa lakabu hiyo. Athari hizo hutokana na sifa za kimwili, kinasaba, kitabia au kimatendo ayafanyayo mtu aliyepewa lakabu hiyo. Kutokana na sababu hiyo, mwandishi wa makala aliona kuna haja ya kufanya utafiti ili kuchunguza mchomozo wa usitiari katika lakabu wanazopewa watu mashuhuri na maarufu nchini Tanzania ili kubaini maana za kisitiari ambazo zimefumbatwa na lakabu hizo na dhamira zinazoibuliwa kutokana na matumizi ya lakabu hizo. Kwa kufanya hivi itasaidia kuonesha ni jinsi lakabu hizo zinasawiri uhalisia na ukweli wa kijamii.

Sitiari kwa mujibu wa Kahigi (1994) ni uhamishaji wa maana kutoka kitu au dhana moja hadi kitu au dhana nyingine. Vikoa vya maana vinavyohusika katika uhamishaji huu huwa vinatofautiana angalau kwa sifa ya kisemantiki moja ya msingi. Kinachohamishwa ni tabia, umbo au kazi ya kitu kwa kuihusisha na tabia au umbo au kazi ya kitu kingine (taz. Lakoff & Johnson, 1980). Katika kufafanua dhana ya sitiari, Jilala (2016) ametumia mfano wa *Juma ni simba*. Anasema "katika mfano huu, hatumaanishi kuwa *Juma* amegeuka kuwa *simba* yaani mnyama; bali sifa za *simba* zinahamishiwa kwa *Juma*. Kwani, *simba* ana sifa ya ukali. Kwa hiyo, ukali unaonasibishwa na simba unahusishwa na ukali wa *Juma"* (Jilala 2016: 165). Muundo wa sitiari una vipengele vitatu: kizungumzwa, kifananisho na kiungo (Lakoff & Johnson, 1980; Kahigi 1994). Kizungumzwa ni kitajwa, ambapo katika mfano wetu, ni *Juma*; kifananishi ni kitu kinachohusishwa na kizungumzwa na katika mfano wetu ni *Simba*, na kiungo ni tabia au sifa zinazounganisha kizungumzwa na kifananishi hapa ni sifa ya ukali. Sitiari hulinganisha kati ya watu na vitu vingine kana kwamba ni sawa. Tazama mistari katika shairi lifuatalo:

> Mama yangu wewe ni nguzo maishani mwangu ni taa
> imulikayo mbele yangu mawazo yako mamaa
> yaniongoza maisha yangu yooote (Jilala, 2008).

Katika shairi hilo tunaona kuwa mtunzi ametumia sitiari 'nguzo' na 'taa' kumwelezea mama na sifa zake. Hapa haimaanishi kuwa, mama amegeuka kuwa nguzo au taa bali zile sifa za nguzo na taa zinahamishiwa kwa mama. Yaani, nguzo ina sifa ya kutoa msaada, mtu anapoegama au kushikilia nguzo humpa msaada. Taa hutoa mwanga, humulika giza na kuleta nuru. Kwa hiyo, sitiari 'taa' na 'nguzo' zimetumika kuonesha umuhimu wa mama katika malezi ya mtoto (taz. Jilala, 2008).

Kimsingi kuna sitiari za aina tatu; sitiari pana, changamano na sahili (Kahigi, 1995). Kahigi pia anafafanua kuwa sitiari sahili ni sitiari ya moja kwa moja na ina kifananishi kimoja, sitiari changamano huwa na vifananishi viwili au zaidi vinavyochangia kutoa dhana mbalimbali juu ya kizungumzwa. Sitiari pana ni ile inayojengwa na semi nyingi za kisitiari na inaweza kuwa sehemu ya shairi, hadithi au tamthiliya au inaweza kuwa msingi na kiunzi cha muundo wote wa shairi, hadithi, au tamthiliya. Sitiari pana hujengwa na sitiari nyingine kama vile sitiari sahili na sitiari changamano. Aidha, tamathali nyingine za semi hutumika katika kujenga sitiari pana. Jilala (2008) anatoa mfano wa kazi za fasihi ambazo zimeundwa kwa sitiari pana ni *Rosa Mistika* (1971), *Nguzo Mama* (1982), *Morani* (1993), *Mashetani* (1971), *Ngoma ya Ng'wanamalundi* (1988) na mashairi ya muziki wa kizazi kipya.

Sitiari moja inaweza kuashiria maana zaidi ya moja katika muktadha na wakati fulani. Mfano, 'ngoma' huweza kuashiria UKIMWI katika muktadha wa ugonjwa na pia huweza kuashiria mwanamke katika muktadha wa mapenzi (Jilala, 2008 & 2010/2011). Vilevile, sitiari zaidi ya moja huweza kubeba maana moja, mfano ngoma, umeme, miwaya zote huashiria UKIMWI (Jilala, 2008).

Kutokana na uelewa huo wa dhana ya sitiari, na pia ndani ya jamii tumekuwa tukisikia watu mashuhuri na maarufu wakipewa ama kujipa lakabu kama vile: mwamba, jiwe, chuma, simba, tembo, na chui. Tujiuliza iwapo lakabu ambazo wanapewa ama kujipa watu mashuhuri na maarufu zinabeba maana za kisitiari? Je, kuna dhamira zozote ambazo zimefumbatwa na sitiari hizo? Hivyo, maswali hayo yalichochea utafiti na uandishi wa makala haya ili kuibua maana na dhamira ambazo zinajitokeza katika sitiari za lakabu za watu mashuhuri na maarufu.

Kwa ujumla makala haya yamegawanyika katika sehemu kuu tano; ambapo sehemu ya kwanza ni utangulizi, sehemu ya pili inahusu mapitio ya kazi tangulizi na mkabala wa kinadharia uliotumika katika utafiti huu. Sehemu ya tatu ni methodolojia ya utafiti. Sehemu ya nne ni ndiyo kiini cha makala hii, imejikita katika kuwasilisha data, kuchambua data na kujadili mchomozo wa usitiari katika lakabu za watu mashuhuri na maarufu, na sehemu ya tano ambayo ni mwisho inatoa hitimisho la Makala haya.

**Tafiti kuhusu Majina**

Sehemu hii inabainisha na kujadili maandiko mbalimbali yanayohusiana na mmakala hii ambayo yamechunguza utoaji wa majina ya watu. Maandiko hayo yamegawanyika katika makundi makuu matatu; ambayo ni Tafiti za majina katika bara la Ulaya, tafiti za majina katika bara la Afrika na tafiti za majina nchini Tanzania. Yafuatayo ni baadhi ya maandiko ambayo mwandishi aliyapitia:

**Tafiti za Majina katika Bara la Ulaya**

Majina ya watu yana nafasi kubwa ya kubainisha nafasi maalumu za wanajamii. Nagy (2010) katika utafiti alioufanya kwa Wacheki huko Jamhuri ya Cheki, aligundua kuwa watu huweza kutambulika nafasi zao kupitia majina. Amebainisha kuwa kimaana jina ni utambulisho wa familia ya mwanajamii. Ameendelea kusema kuwa wanajamii hutumia jina la ukoo ama jina la tatu (surname) kama utambulisho wao. Vile vile amedai kuwa jina ni alama inayosawiri utambulisho na haki ya kutambulika kama mwanajamii wa jamii fulani. Adams (2010) katika utafiti wake wa majina ya watumwa waliomilikiwa na Waingereza amebainisha kuwa ilikuwa ni jambo la kawaida kwa Waingereza kuwabadilisha majina watumwa waliowamiliki. Kwa mfano watumwa wa kike waliwaita "Hagar Blackmore" neno hili ni sinonimia ya neno "Negro" yaani "ngozi yenye kiza". Kwa ujumla utafiti huu unadhihirisha kuwa majina hata katika jamii za Ulaya hubeba maana na hutumika kama wutambulisho wa mtu ndani ya jamii.

**Tafiti za Majina katika Bara la Afrika**

Watafiti mbalimbali katika nchi za Afrika wamefanya utafiti kuhusu majina baadhi yao ni Chulk (1992), Ota (2002), Dawling (2004), Kofi (2006), Agyekum (2006) na James (2011). Inasemekana majina wakati mwingine hutolewa kufuatana na matukio na mambo mbalimbali yanayotokea katika jamii. Kwa mfano Agyekum (2006) ambaye alifanya utafiti kuhusu majina ya watu wa kabila la Akan nchini Ghana aligundua kuwa watu wa kabila la Akan huwapa watoto majina kulingana na siku ya kuzaliwa, familia 10 aliyozaliwa, tukio la tohara (jando), athari za kimaumbile, kama watoto wamezaliwa pacha (wawili ndani ya mimba moja), dini, majina ya kimiujiza, majina yanayotokana na mafanikio, majina ya vijembe na methali (mafumbo), majina ya umbo la mwili wa mtoto aliyezaliwa na majina ya ukoo. Utafiti huu utasaidia kugundua maana na mazingira yanayopelekea watu kupewa majina. Chulk (1992) alitafiti majina ya watu wa Naijeria ambapo alieleza kuwa kawaida watu hupewa majina kutokana na matukio fulani, au vitu vikubwa vya kushangaza, au siku, na Juma mtu alilozaliwa. Mfano "Aiende" Kiyoruba lina maana ya "tuliyekuwa tumemuomba/subiri". Jina hili limetokana na familia ambayo muda mrefu haijapata mtoto wa kiume.

Mfano, James (2011) ambaye alitafiti kuhusu maana za majina ya watu wa kabila la Lulogoli liliopo magharibi ya Kenya na aligundua kuwa kabila hilo hutoa majina kwa kufuata mikabala miwili

ya kimaana katika majina ya watu wa kabila la Lulogooli. (i) Mkabala wa maana halisi (ii) Mkabala wa maana kimatilaba. Alitoa mfano wa jina Ambura analoitwa mtoto wa kiume aliyezaliwa wakati wa mvua na jina "imburani" huitwa mtoto wa kike anaezaliwa wakati wa mvua. Utafiti huu umemsaidia mtafiti kubaini maana za majina tofauti zinazojitokeza kati ya majina ya wanawake na majina ya wanaume katika jamii ya Wajita. Pia umesaidia kugundua tofauti ya kimaumbo kati ya majina ya wanawake na wanaume katika jamii ya Wajita.

**Majina Nchini Tanzania**

Utafiti kuhusu majina nchini Tanzania umefanywa na wataalam mbalimbali baadhi yao ni Muzale (1998), Rubanza (2000), Schotsman (2003), Msanjila na wenzake (2009), Manyasa (2010), Buberwa (2010), Seif (2011) na Mapunda (2014). Kwa mfano, Schotsman (2003) ameelezea historia ya maana ya majina ya mahali katika jiji la Dar es salaam. Utafiti wake ulijikita katika kuchambua majina ya vituo vya daladala na majina ya mitaa/kata. Alibaini kuwa majina ya vituo vya mabasi yanatokana na majengo kama shule hospitali, kanisa, watu maarufu, shughuli zinazofanywa na watu katika eneo hilo. Pia mwelekeo wa kituo kilipo kwa mfano, njia panda kwa Kawawa. Kituo hiki kipo njia inayoelekea kwa Kawawa. Pia anaeleza majina ya mitaa yanatokana na mimea iliyopo katika sehemu hiyo, lugha za asili mfano 'Mwananyamala' maana yake ni 'mtoto usilie', ambalo ni neno la Kizaramo lililotolewa na wanawake walioishi awali katika eneo hilo kutumia usemi huu wakati wakibembeleza watoto wanapokuwa katika shughuli zao za shambani. Majina mengine hutolewa hutokana na maeneo ambayo yanashabihiana mfano 'Mawenzi' ya Dar es Salaam ni eneo lenye mteremko kama mteremko ulioko 'Mawenzi' ya Kilimnjaro.

Msanjila na wenzake (2009) wakielezea majina ya familia wamebainisha kwamba, majina mengi hutolewa kwa lugha inayozungumzwa na jamii husika, hivyo kubeba maana inayotokana na utamaduni wa mazingira ya jamii hiyo. Kwa mfano: (i) Matonya - amezaliwa wakati mvua inanyesha. Hutumiwa kwa wanaume tu. (ii) Mamvula - amezaliwa wakati mvua inanyesha. Hutumika kwa wanawake tu. (iii) Mazengo - amezaliwa wakati wa kukata miti ya kujengea nyumba. (iv) Matika - amezaliwa wakati vyakula shambani vimeiva, watu wanavuna. (v) Manzala - amezaliwa wakati wa njaa, watu hawana chakula cha kutosha. (vi) Chonyamagulu - tukio la njaa lililotokea mwaka 1860 ambalo lilidhoofisha miguu ya watu kiasi cha kuwafanya washindwe kutembea. (vii) Magubika - tukio la njaa lililotokea miaka ya 1888 na 1889 lililofanya watu wafunike vyungu vya kupikia kwa sababu kulikuwa hakuna kitu cha kupika. (viii) Mutunya - tukio la njaa ambalo liliwapa watu shida sana ya kutafuta chakula sehemu mbalimbali hata wakadiriki kusafiri nje ya mkoa wa Dodoma. Njaa hii ilitokea miaka ya 1913.

Manyasa (2010) alitafiti majina katika jamii ya Wasukuma na alieleza sababu zitumikazo kutoa majina ya watu katika jamii hiyo. Amebainisha kwamba, majina katika jamii ya Wasukuma hutolewa hutokana na matukio kipindi cha kuzaliwa mtoto, yanaweza pia kutokana na magonjwa makali yanayompata mtoto kipindi cha kuzaliwa. Kwa mfano 'Mboku' ni jina ambalo hupewa mtoto mwenye uoni hafifu. Pia jina linaweza kutokana na hadhi ya mtu, mfano 'Mtemi' hupewa mtoto wa kiume aliyezaliwa kipindi cha utawala (mtemi) maarufu. Vilevile, matukio yaliyokuwepo katika kipindi cha kuzaliwa mtoto, mfano mtoto aliyezaliwa wakati wa vita huitwa 'Nshilikale'. Mtaalamu huyu anafafanua kwamba utoaji wa majina unatofautiana kati ya jamii moja na jamii nyingine. Utafiti huu umempatia mtafiti muongozo wa kugundua kuwa majina hutolewa kwa sababu maalum za kiitikadi katika jamii na matendo ya jamii husika.

Seif (2011) anaeleza asili ya mitaa iliyopo Morogoro; kwa mfano, Gairo asili yake ni 'Kigairo' (yaani sehemu ya kugawiana (vitu) sehemu hiyo hapo zamani watemi waliitumia kugawiana meno ya ndovu, Wakaguru walikuwa wanasema tu "chikututa chigairo" tunakwenda 14 sehemu ya kugawiana. Baadaye likawa gulio (soko la jumla na reja reja). "Misingisi" ni jina linalotokana na mti wa Kikaguru unaoitwa msingisi. Kutokana na maelezo hayo yote ni dhahiri kwamba majina ya mahali yana asili maana na sababu za kuitwa hivyo. Baada ya kuangalia maana ya majina ya mahali na asili ya majina ya mitaa, tutaangalia majina ya watu na mazingira yake ambayo ndio kiini cha utafiti wetu. Mapitio

haya yalimsaidia mtafiti kuongeza uelewa juu ya majina ya asili ya watu wa jamii mbalimbali na Wajita.

Baada ya kutalii baadhi ya tafiti ambazo zimefanyika kuhusu majina tulibaini kuwa, tafiti na makala nyingi zimezungumzia lakabu mbalimbali lakini wahakujikita katika kulenga kuchunguza mchomozo wa usitiari katika lakabu za watu mashuhuri na maarufu nchini Tanzania. Kwa mantiki hiyo, tuliona lakabu wanazopewa au kujipa watu mashuhuri na maarufu yanahitaji kuchunguzwa ili kubaini maana na dhamira zilizofungamana na majina hayo. Vilevile, tafiti tangulizi na machapisho kuhusu majina zilituongoza katika mjadala wa makala haya. Aidha, nadharia na kanuni zilizobainishwa katika tafiti zingine zitatuongoza katika mjadala wa makala haya.

**Mkabala wa Kinadharia**

Utoaji wa majina ya watu, athari na dhima zake zimejadiliwa na kufafanuliwa na wataalamu mbalimbali wa isimujamii, wakiwamo Omary (1970), Chulk (1992), Mulokozi (1996), Rubanza (2000), Schotsman (2003) na Agyekum (2006) na Adams (2010), kwa kuwataja wachache. Kila mmoja kati ya wataalamu hawa ametumia nadharia yake kulingana na dhamira aliyokusudia katika dhana ya utoaji wa majina katika jamii. Hata hivyo, wote wanaelekea kukubaliana kwamba utoaji wa majina ya watu na lakabu hufanyika kwa kuzingatia vigezo maalumu kama vile sifa za kimwili, kinasaba na kitabia au kimatendo ayafanyayo mtu aliyepewa jina. Pamoja na kuwapo nadharia mbalimbali zinazotumika katika kuchunguza majina na lakabu za watu, uwasilishaji na uchambuzi wa makala haya umefanyika kwa kutumia nadharia mbili; *Nadharia ya Jumuishi* ya (Giles, 1979) na *Nadharia ya Semiotiki* (Saussure, 1976) kama anavyonukuliwa na Wamitila, (2003). Sababu ya kutumia nadharia mbili katika uchunguzi na mjadala wa makala haya ni kwamba tuliona nadharia hizi zinategemeana na kukamilishana na hivyo zinafaa katika kutuongoza kwenye mjadala wa makala haya.

Nadharia Jumuishi ya Giles (1979) inafafanua kwamba utambulisho wa mtu au jamii ni mchakato unaoendelea ambao kimsingi unahusisha vibainishi vingi vinavyodumishwa na jamii lugha ambayo huunda kiini cha utambulisho wa jamii. Msingi wa nadharia jumuishi unazingatia fasili ya jamii lugha inayosema: "Jamii inaundwa na wale watu wanaojiona na kujitambua wenyewe" (Giles, 1979: 253). Fasili hii ya jamii lugha, mbali na kuwa msingi wa nadharia hii jumuishi pia ni msingi wa maana halisi ya utambulisho. Maana halisi ya utambulisho kwanza ni kuwa jamiilugha yenyewe hujitambua kuwa iko tofauti na jamiilugha nyingine katika masuala msingi kama utamaduni, mila na desturi, imani (dini) chakula, mavazi, uchumi au siasa. Kwa kuwa majina ya watu huathiriwa na utamaduni, mila, desturi, na imani (dini) na kwa kuwa majina ni mojawapo kati ya vibainishi vya jamii tumeamua kumetumia nadharia jumuishi ya Giles ili kuweza kubaini maana, sababu na faida vinavyowaongoza jamii ya Wajita katika kutoa majina ya watu.

Aidha, Nadharia ya Semiotiki (Saussure, 1976) inahusu ishara na mfumo wa ishara katika lugha. Semiotiki inajumuisha uchunguzi, uelewa na utabiri wa maana za ishara na namna zinavyopatikana katika vitu halisi. Kwa ujumla semiotiki ni nadharia inayojishughulisha na utoaji na ufasili wa maana za ishara mbali mbali (James 2011). Waanzilishi wa nadharia ya semiotiki ni mwanaisimu wa ki-Swizi, Ferdinand de Saussure, na mwanafalsafa wa kipragmatiki kutoka Marekani, Peirce (Wamitila, 2003). Kimsingi, nadharia ya semiotiki inashughulikia ishara na uashiriaji (maana zao) katika matini za kifasihi (Scholes 1982; Wamitila 2002). Nadharia ya Semiotiki imetumiwa na mtafiti James (2010) katika utafiti wake wa maana za majina ya watu wa kabila la Lulogooli.

Kwa ujumla, nadharia hizi zilimsaidia mwandishi kuchunguza mchomozo wa usitiari katika lakabu za watu mashuhuri na maarufu katika jamii ya Watanzania. Pamoja na mambo mengine, nadharia Jumuishi na Semiotiki ambazo zimetumika kuongoza uchambuzi na uchanganuzi wa makala hii imetusaidia kubaini, kujadili na kufafanua mchomozo wa usitiari katika lakabu za watu mashuhuri na maarufu katika jamii ya Watanzania. Kupitia Nadharia Jumuishi ya Giles (1979) tuliweza kuubaini fasili ya maana za kisitiari na dhamira ambazo zimefumbatwa na lakabu hizo.

**Methodolojia ya Utafiti**
Data za utafiti huu zilikusanywa kwa kutumia mbinu ya usaili na usomaji makini wa maandiko katika mkoa ya Dar es Salaam baina ya miezi ya Disemba 2021 na Machi 2022. Usomaji makini ulihusisha usomaji wa vitabu, makala, vipeperushi na majarida yanayohusiana na mada ya utafiti huu kutoka kwenye taarifa za mtandaoni kama vile tovuti na wavuti, mitandao ya kijamii na makavazi. Data za usaili zilikusanywa kutoka kwa wanajamii na kisha zilirekodiwa katika kinasa sauti na kunukuliwa kwa maandishi. Sampuli ya kundi hili iliteuliwa kwa njia ya usampulishaji nasibu. Uteuzi wa kundi hili ulitokana na sababu kuwa iliaminika wao ndiyo watu ambao hushiriki katika kutoa lakabu na hivyo wanafahamu sababu na maana za kisitiari za lakabu hizo. Kupitia kundi hili tuliweza kupata data za lakabu za watu maarufu na mashuhuri, sitiari na maana zake na pia dhamira zinazoibuliwa na sitiari hizo.

**Matokeo na Mjadala wa Uchunguzi**
Kama tulivyobainisha hapo awali lengo la makala haya lilikuwa ni kubainisha mchomozo wa usitiari katika lakabu za watu mashuhuri na maarufu nchini Tanzania. Lakabu za watu mashuhuri zilihusisha lakabu za Marais, na lakabu za watu maarufu zilihusisha wasanii wa muziki wa Bongo fleva[1]. Ili kufikia lengo hilo, makala haya yalitumia mbinu ya usomaji makini na usaili kuchunguza sitairi na maana zake katika lakabu wanazopewa watu mashuhuri na maarufu na sitiari na kisha kubaini dhamira zinazotokana na usitiari wa lakabu hizo. Matokeo yalikuwa kama inavyojidhihirisha katika sehemu zifuatazo;

**Usitiari katika Lakabu za Watu Mashuhuri na Maarufu**
Moja ya malengo mahsusi ya makala haya ilikuwa kubainisha lakabu za watu mashuhuri na maarufu nchini Tanzania. Uchunguzi ulijikita katika kuchunguza lakabu za watu mashuhuri ambao ni viongozi wakuu wa nchi (Marais) na lakabu wanazopewa watu maarufu ambao ni wasanii maarufu wa Bongo Fleva. Matokeo ya utafiti yalikuwa kama inavojidhihirisha katika jedwali namba 1 na 2.

**Usitiari katika Lakabu za Marais**
Lakabu zilizochunguzwa katika makala hii ni majina ya kupanga wanayopewa Marais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuanzia awamu ya kwanza mpaka ya sita. Utafiti huu ulibaini kuwa kila Rais aliyeongoza nchi alipewa lakabu yake na wananchi. Lakabu hizo hutolewa kwa kuzingatia sifa za kisiasa, kiutamaduni, kiuchumi, kielimu na kijamii. Hivyo, imekuwa ni hali ya kawaida katika nchi ya Tanzania kila Rais anapewa lakabu inayomtafautisha na wengine. Jedwali namba 1 linawasilisha data hiyo:

**Jedwali Na. 1: Usitiari katika Lakabu za Marais**

| Na. | Jina la Rais | Lakabu ya kisitiari aliyopewa | Maana Asilia | Maana ya Kisitiari |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Julius Kambarage Nyerere | Mchonga meno | Mtu ambaye meno yake yamechongwa | Kiongozi mwenye fasaha ya kusema na ushawishi |
| | | Baba wa taifa | Mzazi wa kiume au kiongozi wa familia | Kiongozi mwasisi au mwanzilishi wa taifa la Tanzania |
| | | Mzee wa kifimbo | Kipande cha mti kinachotumika kuadhibia mtu | Kifimbo kina ashiria utawala wa kiongozi |
| 2. | Ali Hassan Mwinyi | Mzee wa ruksa | Mtu ambae huruhusu kufanyika kila jambo zuri analoshauriwa | Kiongozi aliyefungua mipaka na uhuru, mpole |

[1] Bongo Fleva ni muziki unaoimbwa na vijana (Omari, 2008; Jilala, 2008;

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 3. | Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete | Mzee wa Msoga | Mtu mwenye asili ya kijiji cha Msoga | Kiongozi anayependa kukikuza na kukiendeleza kijiji chao |
| 4. | John Pombe Magufuli | Tingatinga | Chombo kinachotumika kukata milima na miamba katika kutengeneza Barabara | Kiongozi mwenye ujasiri wa kufanya maamuzi magumu |
| | | Mwamba | Jiwe lililoshikana ardhini au kwenye maji ambalo ni gumu sana | Kiongozi imara na madhubuti |
| | | Jiwe | Kipande cha mwamba kilichomeguka | Kiongozi imara na madhubuti, mkali |
| | | Burudoza | Chombo kinachotumika kung'oa miti mikubwa, kubomoa majengo na kuchimbua ardhi | Kiongozi mwenye ujasiri wa kufanya maamuzi magumu |
| | | Chuma | Madini yanayotengenezwa vitu vigumu kama vile nondo, bati, nk | Kiongozi shupavu, imara na madhubuti |
| 5. | Dkt. Samia Suluhu Hassan | Mama | Mzazi wa kike au mlezi wa familia | Kiongozi anayejali na kuwalinda wananchi ili waishi kwa matumaini |

**Chanzo:** Data za Utafiti 2021

Katika jedwali namba 1 hapo juu tulibaini lakabu za viongozi wa nchi Marais sita wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambazo walipoewa na wananchi kwa nyakati tofauti kulingana na utawala wao. Ukichunguza lakabu hizo utabaini kuwa ni majina ya kisitiari ambayo yamebeba maana za kisitiari kuashiria athari na uongozi ambao viongozi hao wameutoa katika jamii. Mchango wao katika maendeleo na ustawi wa nchi kiuchumi, kisiasa, kijamii na kiutamduni. Hivyo, kutokana na data hiyo makala haya yamebaini kuwa sitiari hutumika kuunda majina ya viongozi kwa kuzingatia sifa, tabia, aina ya uongozi na matakwa ya kijamii. Sehemu ifuatayo inajadili kwa kina.

**Lakabu Zitokanazo na sifa**

Makala haya yalibaini kuwa yapo majina ya kisitiari ambayo hupewa viongozi kwa kuzingatia sifa za kiongozi na hivyo majina hayo yanatumika kisitiari kuashiria na kuibua dhamira kutokana na sifa hizo. Mfano sifa za ukali, upole, uchapakazi, ustadi, uimara, ushujaa na uzalendo. Mifano ifuatayo inafafanua sifa ambazo zilibainishwa katika majina ya kisitiari yaliyotolewa kwa viongozi.

**Sifa ya Uchapakazi**

Miongoni mwa sifa zilizojitokeza katika majina ya viongozi ni sifa ya uchapakazi. Tazama mifano ifuatayo;

***Burudoza:*** BAKITA (2017) inafasili burudoza kama chombo kikubwa chenye magurudumu bapa ya chuma na jembe mbele ambacho hutumika kuchimbia ardhi, kubomoa majengo na kutengeneza barabara. Jina hili limetumika kisitiari kuwasilisha sifa ya uchapakazi kwa kiongozi.

Wahojiwa walitaja lakabu Burudoza kuwa ni jina alilopewa Hayati Dkt. John Pombe Magufuli aliyekuwa Rais wa awamu ya tano wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania. Jina hili lilitolewa kipindi cha kampeni za uchaguzi mwaka 2015 na mwaka 2020 wakati akigombea Urais ili kumnadi kiongozi huyu kwa wananchi kuwa ni kiongozi mchapakazi ambaye hawezi kushindwa kitu katika kuleta maendeleo ya nchi.

Wakati wa utafiti wahojiwa walisema wananchi walimpa jina hilo kuashiria sifa ya 'uchapakazi' na pia kwa kuzingatia kauli mbiu yake ya 'hapa kazi' tu iliwafanya wananchi kumpa jina hilo ili kujenga dhana ya kiongozi mchapakazi.

Jina 'burudoza' limetumika kisitiari kwa kuchukua sifa za Burudoza na kuzihamishia kwa John Pombe Magufuli ambaye anafananishwa na kifaa kinachotumika katika kubeba vitu ama kuhamisha vitu vizito ambavyo vilivyoshindikana kutoka eneo moja kwenda eneo lingine kwa kutumia mikono ya binadamu. Hivyo, sitiari hii imetumika kuashiria dhana ya uimara, umahiri na ushujaa wa kiongozi katika kutekeleza majukumu yake na kupambana na hali duni ya maisha ya jamii na hivyo kuibua dhamira ya uchapakazi. Kupambana na rushwa, ufisadi, ujinga na umaskini ndani ya jamii. Wahojiwa walieleza dhana ya 'kutumbua majipu' ambayo ililenga kujenga sifa na tabia ya uwajibikaji ambapo hakuna kila aliyeonekana hatimizi wajibu wake aliondolewa katika madaraka yake.

***Chuma:*** Wahojiwa walibainisha jina 'chuma' ambalo wananchi walimpa Dkt. John Pombe Magufuli na yeye mwenyewe alizoea kujita. Kwa mfano kupitia mitandao ya kijamii tuliweza kubaini video ya moja ya hotuba zake ambapo anasema "naomba niwaambie Watanzania mna kiongozi chuma…tena chuma kweli kweli… ni bora nipoteze uhai wangu lakini nipiganie maslahi ya nchi yangu siogopi lolote" msisitizo katika kauli yake kuhusu jina la 'chuma' ambalo limetumika kisitiari kuibua dhamira ya ujasiri, ushujaa na uimara wa kiongozi huyo. Aidha, jina hili linasadifu ujenzi wa jamii mpya ambao umejiegemeza katika uongozi imara wenye kujali na kulinda maslahi ya taifa kiuchumi, kijamii, kisiasa na kiutamaduni.

***Jembe:*** Jembe ni kifaa kinachotumiwa na mkulima katika kulima na kupalilia shamba na kupitia jembe mkulima huweza kuzalisha mazao na mali. Utafiti huu ulibaini kuwa Dkt. John Pombe Magufuli alipewa jina 'jembe' ambalo limetumika kisitiari kuashiria sifa ya uongozi, imani na utegemezi wa wananchi na nchi juu ya kiongozi huyo. Taifa linamtegemea kama nguzo ya kufikia ajenda na dira ya taifa ya mafanikio na maendeleo endelevu ya taifa, kuinua uchumi na hali ya maisha ya Watanzania kutoka katika umaskini na kukuza uchumi wa taifa. Hivyo, matumizi ya neno 'jembe' kama jina la Rais limetumia kisitiari kuonesha kuwa Rais ni jembe ambalo Wananchi na nchi inalitegemea katika kufikia malengo ya maendeleo endelevu ya jamii kiuchumi, Kisiasa, Kijamii na kiutamaduni. Aidha, uongozi na matendo ya Magufuli yalimpa sifa ya kuitwa jembe la watanzania. Kwa kutumia kauli mbiu yake ya 'hapa kazi' tu ambayo pia inasawiri dhamira yake ya kuhakikisha analeta maendeleo kwa wananchi. Hii ina maana kwamba alitumia nafasi yake kufufua uchumi, kujenga miundo mbinu ambayo inarahisisha maendeleo ya nchi kama vile barabara, reli ya umeme, madaraja, kulinda raslimali za nchi kama vile madini, wanyama katika hifadhi za utalii na kuboresha huduma za elimu, huduma za kijamii katika sekta za afya na sekta zingine za kijamii. Aidha, aliweza kuimarisha sekta ya utalii, kukuza na kuongeza tija katika viwanda kwa kauli mbiu yake ya "Tanzania ya viwanda"

Jina "***Mwamba***" kwa manaa ya kawaida ni kwamba mwamba hauwezi kuvunjika ama kuanguka kirahisi. Mwamba huwa ni jiwe imara lisilo na kuteteleka. Matumizi ya jina "mwamba" ni ya kisitiari ambayo sifa za mwamba zinahamishiwa kwa Rais kurejelea uimara, nguvu na ushujaa wa John Pombe Magufuli

Jina "***Jiwe***", utafiti huu ulibaini kuwa jina 'jiwe' lilitumika kumrejelea Rais Magufuli. Jina 'jiwe' ni la kisitiari ambapo sifa za 'jiwe' zinahamishiwa kwa Magufuli kwa kuzingatia utendaji kazi na uongozi wake. "Jiwe" limetumika kuashiria uimara, ujasiri na ushujaa katika uongozi wake. Jiwe haliwezi kuvunjwa na mtu, ni imara. Hivyo, uongozi wa Rais uliojaa ujasiri, ushujaa na uimara uliwafanya Watanzania wamwite 'jiwe'. mtu imara, jasiri na asiyeteteleka mwenye msimamo thabiti.

Wahojiwa walibainisha kuwa miongoni mwa sifa zilizomfanya apewe jina ‘jiwe’ ni kutokuwa na hofu. Hofu ambayo katika hotuba zake aliikemea na kuwaasi Watanzania kuondoa hofu na kuchapa kazi. Mfano katika utafiti huu tulibaini video ya moja ya hotuba yake akitoa kauli kuwa “…ndugu zangu hofu ni mbaya…ondoeni hofu na mchape kazi” kauli hii inasadifu aina ya kiongozi na uongozi wake. Hivyo, kupitia kauli hii jina la ‘Jiwe’ linadhihirisha ushujaa, ujabari na uongozi imara usiokuwa na hofu katika kutetea na kulinda maslahi ya nchi. Aidha, vitendo vya kupambana na rushwa hadharani kama vile kutumbua viongozi wasio waadilifu na wachapa kazi. Kuwachulia hatua kwa wakati viongozi wala rushwa na mafisadi bila kujali nguvu na uwezo walionao. Hivyo, kiongozi huyu aliitwa “jiwe”

**Sifa ya Mama**

Katika kujenga nafasi ya mwanamke katika jamii, jina la mama ambalo huitwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Samia Suluhu Hassan linasadifu nafasi ya mwanamke katika ukombozi wa kiuchumi na maendeleo endelevu ya nchi. Jina “mama” limekuwa likitumika kila sehemu mfano mtu anaweza kusema Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mama yetu…” Kwa hiyo, jina mama limekuwa likitumika kumrejelea Rais Samia Suluhu Hassan. Hii ni tofauti na Marais wengine waliotangulia ambao haikuwa rahisi kusikia mtu akiita Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania baba …...

Kwa muktadha huo neno ‘mama’ lina nguvu na linatumika kisitiari kudhihirisha matumaini ya wananchi kwa Rais Mwanamke. Sifa ya mama kwa mtoto ambayo ni ulezi, upendo na huruma inahamishiwa kwa Rais. Aidha, majukumu ya mama kwa familia yanasawiri jina hili.

**Mama** jina mama linatumika kisitiari kama ishara ya kurejelea tumaini jipya katika jamii. Wakati wa usaili wahojiwa walieleza ni kwa nini wanamuita Rais mama na haya yalikuwa majibu yao “Mama ni mzazi, mlezi, upendo, na kiongozi imara wa familia, Mama ni mzalendo kwa familia yake hawezi kuikimbia familia na watoto wake. Mama yupo tayari kufia wanawe na familia yake katika magumu na furaha”. Hivyo, neno ‘mama’ hutumika si kwa sababu Rais ni mwanamke bali ni sitiari inayoashiria malezi, jukumu la uzazi na ulezi, huruma, upendo, kujali, uongozi na thamani ya mama kwa nchi. Watanzania hubeba matarajio na tumaini jipya la uongozi wa mama kama mzazi, mlezi na kiongozi imara wa familia. Ujenzi wa nchi na uchumi wa nchi umejiegemeza katika kiongozi imara, mvuilivu, mwadilifu na mweye uzalendo. Hivyo, sitisari hii imebeba dhamira pana ya Rais Samia katika kujenga uchumi na maendeleo ya nchi ya tanzania katika nyanja zote. Mama husafiri kwenda huku na kule kutafuta chakula cha watoto na familia yake. Hii inadhihirishwa na hotuba ya Rais Samia alipoapishwa na kuonesha dhamira ya dhati kama kiongozi mwanamke katika kujenga jamii imara yenye uchumi imara na thabiti.

Jina la ***baba wa taifa*** alipewa J.K. Nyerere kutokana na sifa ya kuwa kiongozi wa kwanza wa nchi, aliongoza harakati za kudai uhuru wa Tanganyika, kuliongoza taifa la Tanzania kwa muda mrefu zaidi. Sifa hizi zilitumika kisitiari kumpa J. K. Nyerere jina la baba wa taifa.

Jina la ***mchonga meno*** ni jina ambalo limetokana na sifa ya J. K. Nyerere ya meno yake ya mbele kuachana kwa nafasi kubwa na hivyo kushairia kuwa alikuwa amechonga meno.

**Lakabu Zinazotokana na Mabadiliko ya Kiuchumi**

Majina ya kisitiari kwa viongozi yalitolewa kulingana na sifa na mchango wa kiongozi katika kuleta mabadiliko ya kiuchumi. Mfano Rais Mstaafu wa Awamu ya Pili Alhaji Ali Hassan Mwinyi alipewa jina la “Mzee wa Fursa’ jina hili ni la kisitiari ambalo linaashiria ni kiongozi aliyefungua fursa za kiuchumi ndani ya nchi. Jina hili lilitolewa kutokana na uhalisia wa kihistoria ambapo nchi ya Tanzania ilikuwa katika kipindi kigumu kiuchumi na hivyo biashara za ndani na nje ya nchi zilikuwa hazifanyiki. Wananchi walikosa mahitaji ya msingi kutokana na hali ngumu ya kiuchumi. Baada ya Ali Hassan Mwinyi kuingia alifungua fursa za kiuchumi, kisiasa, kiutamaduni na kijamii na hivyo wananchi walimpa jina la mzee wa ruksa. Kila kitu kiliruhusiwa ili mradi usivunje sheria za nchi.

**Lakabu zitokanazo na tabia ama Mazoea**

Utafiti huu ulibaini kuwa lakabu walizopewa viongozi zilitokana na tabia ama mazoea fulani ambayo kiongozi huyo aliizoea. Kwa mfano jina la Mzee wa kifimbo alipewa J.K. Nyerere kwa sababu ya

tabia ya kushika kifimbo chake hata anapokuwa katika matukio maalumu. Hivyo wananchi walimpa jina la Mzee wa Kifimbo kuashiria mtu aliyezoea kushika fimbo.

**Usitiari katika Lakabu za Wasanii Maarufu**
Katika kipengele hiki tunajikita katika kuchunguza lakabu wanazopewa ama kujipachika watu maarufu hususan Wanamuziki. Na utafiti wetu ulijikita katika kuchunguza majina ya Wanamuziki maarufu nchini Tanzania ambao ni Naseeb Abdul Juma (Diamond Plutnumz), Raymond Shaban Mwakyusa (Rayvan) na Rajab Abdul Kahali (Harmonise). Data zilikusanywa kupitia mitandao ya kijamii kama vile instagram, facebook na Whatasap. Vile vile majina mengine yalikusanywa kupitia redio, televisheni na magazeti. Wakati wa usaili wahojiwa walitakiwa kutaja lakabu za wasanii hao na maana zake. Matokeo yalikuwa kama ifuatavyo:

**Jedwali Na. 2: Usitiari katika Lakabu za Wasanii Maarufu wa Bongo Fleva**

| **Na.** | **Jina la Msanii** | **Lakabu ya kisanii** | **Maana Asilia** | **Maana ya Kisitiari** |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Nasibu Abdul Juma | Simba | Mnyama anayejulikana kwa sifa ya ukali na ufalme wa Wanyama wengine katika hifadhi | Mfalme katika tasnia ya muziki, mwenye nguvu na uwezo mkubwa, mkali |
| | | Diamond | Madini ya almasi | Uzuri na thamani |
| | | Asali ya Warembo | Ni kitu kitamu | Mwanaume anayependwa na wanawake wazuri |
| | | Dangote, | Jina la mtu Tajiri na maarufu ni mwekezaji na mmiliki wa kiwanda cha simenti kilichopo Mtwara | Utajiri na Mali |
| | | Chibu Dangote | Jina la kitoto la Naseeb | Utani |
| 2. | Rajabu Abdul Kahali | Harmonise | Mtu anayetangamanish a watu katika jamii | Mwanamuziki mwenye nguvu za kuleta utangamano katika jamii. |
| | | Tembo | Mnyama mkubwa anayeishi katika hifadhi za Wanyama | Mwanamuziki mkubwa na mwenye nguvu katika tasnia |
| | | Jeshi | Ni tasnia iliyo na dhamana ya kulinda nchi na mipaka yake | Mpambanaji katika vita vya Sanaa |
| | | Konde boy | Kijana wa Kimakonde | Umaskini na mahali alipotoka |
| 3. | Rayvan | Chui | Mnyama mkali anayeishi kwenye mbuga za Wanyama | Mpambanaji katika vita vya Sanaa |

**Chanzo:** Data za Utafiti 2021

Katika jedwali namba 2 hapo juu tunabaini lakabu za wasanii ambazo hupewa na jamii ama kujipa wao wenyewe. Lakabu hizo zimetumika kistiari na maana za majina hayo zinabeba ishara na taswira tofauti kulingana na mwanamuziki. Utafiti huu ulibaini kuwa majina ya kisitiari ambayo wasanii hujipa ama kupewa yanaashiria dhana zifuatazo; dhana ya majigambo, dhana ya majina ambayo msanii anajipa kwa ajili ya majigambo kwa ajili ya kazi yake, kipaji na uwezo, majina ambayo msanii hupewa ama kujipa kutokana na sifa yake nzuri ama mbaya ndani ya jamii, majina ambayo msanii hupewa kama jina la utani. Kwa mfano Naseeb Abdul kujipa lakabu ya ‘simba’

inaashiria sifa za mnyama simba anazihamishia kwake simba ni mnyama mwenye 'nguvu' na 'mtawala' wa porini ambapo Wanyama wengine humuogopa. 'Nguvu' na 'utawala' inaashiria nguvu, utawala, uwezo na ubingwa katika ushindani wa biashara ya Muziki. Hii ina maana kuwa Naseeb Abdul ni msanii mkubwa mwenye nguvu na mtawala katika tasinia na biashara ya muziki. Kwa mujibu wa mahojiano yake na gazeti la msanii anaeleza kuwa yeye ni hodari, haogopi kitu n ani mwenye kujituma katika kazi yake huifanya kwa nguvu, uwezo na weledi. Anasema akiingia kwenye jukwaani anafanya vitu vikubwa na akiimba anaimba akitoa wimbo anatoa wimbo mkali unaotikisa (…). Lakabu ya simba pia inatumika kisitiari kurejelea sifa ya mnyama simba ya kuwa na wanawake wengi hii inajitokeza pia katika wimbo wake wa *Sikomi* kama anavyosema katika mistari hii:

(i) "…Moyo unanambia nasibu sasa mapenzi basi
Ila nang'ang'ania najaribu kuipinga nafsi
Lizer ananiambia simba mapenzi basi
Ila nang'ang'ania
Nikiumizwa na huyu kesho nna mwingine"

Dondoo namba 1. Hapo juu inaonesha jinsi Naseeb anavyoshughulishwa na suala la mapenzi na wanawake. Kwa upande mwingine lakabu 'Diamond' hii ni madini ya almasi ambayo yana sifa ya 'uzuri' na 'thamani'. Uzuri na thamani zimebeba ishara ya uzuri na thamani ya kipaji chake cha uimbaji, nyimbo na muziki wake. Jina la asali ya warembo linaashiria 'mapenzi' hii ina maana kuwa Naseeb Abduli anapendwa na wanawake na amekuwa na mahusiano ya wanawake wengi wazuri ambao yanajithibitishwa na yeye mwenyewe katika mitandao ya kijamii. Jina hili alipewa baada ya kuwa na mahusiano na wasichana mbalimbali Tanzania, Uganda na Kenya.

Dangote kwa mujibu wa Radio Jambo (https://radiojambo.co.ke/burudani/dakia-udaku/2022-07-19-diamond-afichua-asili-ya-jina-lake-la-utani-chibu-dangote/) Naseeb alifichua siri ya kujiita Dangote kuwa ni njia ya kujigamba kuhusu utajiri wake mkubwa alionao kutokana na mafanikio ya Muziki. Aidha, alieleza kuwa alipokuwa mtoto hakuweza kulitamka vizuri jina lake 'Naseeb' na badala yake alilitamka kama 'Chibu', hivyo likawa jina lake la utani.*"Chibu ni Naseeb. Jina langu halisi ni Naseeb. Nikiwa mtoto mdogo singeweza kutamka jina Naseeb. Nilikuwa najiita Chibu. Nikiulizwa jina langu nilikuwa nasema Chibu,"* Diamond alisema.

**Diamond Platnumz**

Nasseb alieleza sababu za kujiita Diamond aliposhiriki katika tamasha la muziki la Coke Studio Afrika kusini ambapo alitengeneza wimbo uliowavutia wengi kwa kushirikiana na Cassper Nyovest, wimbo unaitwa My Heart. Alifanya mahojiano na waandaaji na kueleza jinsi alipopata jina lake la sanaa 'Diamond Platnumz.' Alisema chanzo ni alipokuwa akiimba rafiki zake mtaani walikuwa wakimwambia kuwa ana kipaji kizuri cha kuimba na siku akipata mtu wa kukiendeleza, ataweza kuwa mwenye thamani kama Diamond. Kipindi hicho walianza kumuita Diamond na kwa vile hakukuwa na msanii aliyetumia jina hilo kwa kipindi hicho aliamua kulitumia na kuanza kujita Diamond. Naseeb alisema Diamond lina maanisha mtu mtanashati mwenye swaga, mwenye muonekano wa kuvutia na mtu wakupendeza kila mara (https://www.udakuspecially.com/...diamond-aelezea-sababu-ya-kujiita-jina.html).

Kwa upande mwingine data za makala haya zinaonesha kuwa jina Jeshi na Tembo ni majina ambayo yametumika kisitiari kumrejelea msanii Rajab (Harmonize). Jeshi ni taasisi inayofanya kazi ya kupambana na kulinda mipaka ya nchi, kupigana vita pale panapokuwa na migogoro ya kidiplomasia. Katika utafiti huu tulibaini kuwa lakabu hii imetumika kisitiari kuashiria 'vita', 'mapambano' na 'ushindani' katika kutafuta Maisha na mafanikio kupitia sanaa na biashara ya muziki. Hili linajidhihirisha kutoka katika wimbo wa *Jeshi* ulioimbwa na Harmonize. Tazama mfano kutoka katika misitari ya wimbo wa *Jeshi*:

(ii) "… One love kwa wanangu wa kitaa nyie ndo mnanunua CD
Two love kwa wanafiki wa insta mnanifanya niongeze bidii
Three love kwa Master na Lita Mlinifanya hasira izidii

Four love njia ngumu nilizopita mkanipa na jina mkasema niitwe
Jeshi! Konde boy Jeshi
Na hizi wananiita tembo
Jeshi! Hata we ni jeshi!
Yaani kama huna pigo za kirembo
Ni jeshi! Konde Boy Jeshi!
Yaani wanangu wananiita Tembo
Jeshi! Hata we ni jeshi! …"

**Chanzo: Data za Utafiti, 2022**

Ukichunguza mistari hiyo kutoka katika wimbo wa Harmonize utaona kuwa msanii anabainisha kuwa shabiki zake ndiyo waliompa jina la 'Jeshi' hii ni kutokana na njia ngumu alizopitia. Sifa ya Jeshi kama taasisi ni kutoa mafunzo mazito, magumu, makali na yanayohitaji uvumilivu mkubwa kwa walengwa ili kuandaa watu wakakamavu wenye uwezo wa kupambana. Hivyo, sifa hizi zinaringanishwa na mapambano na harakati za maisha ya kimuziki ya Harmonize anasema 'njia ngumu nilizopita mkanipa na jina mkasema niitwe 'Jeshi'. Pia msanii anazidi kuonesha kuwa kutokana na maisha yake na mapambano aliyonayo katika tasinia ya muziki mashabiki zake wamemuita 'Tembo'. Tembo ni mnyama mkubwa kuliko wanyama wote katika hifadhi za mbuga za Wanyama/porini. Sifa ya ukubwa wa tembo inahamishiwa kwa Harmonize ili kuonesha ukubwa na uwezo wa kipaji chake katika tasnia ya Muziki.

Utafiti huu ulibaini kama ilivyo 'Simba' kwa Naseeb yeye amejipa na kupewa lakabu ya Tembo. Wanyama wote hawa kila mmoja ana sifa zake porini. Wakati wa usaili wahojiwa walibaini kuwa wasanii wapo katika mashindano ya vipaji, uwezo, nguvu na biashara. Kwa hiyo, ili kudhihirisha uwezo na ukubwa wao hutumia majina ya Wanyama kulingana na sifa za Wanyama hao ili kuwasilisha nguvu, uwezo na utawala walionao katika tasinia ya muziki. Hii inajidhihirisha katika majina ya wasanii watatu ambao kila mmoja amechukua majina ya Wanyama wanaojulikana kama wafalme wa mbuga/hifadhi ambao ni Simba, Tembo na Chui.

**Dhamira zinazoibuliwa kutokana Lakabu za Kisitiari**

Makala hii pia ililenga kuchunguza dhamira zinazoibuliwa kutokana na sitiari zinazojichomoza kwenye lakabu za watu mashuhuri na maarufu hususan maraisi na wasanii wa muziki wa bongo fleva. Utafiti huu ulibaini kuwa dhamira zinazojitokeza katika majina yaliyochunguzwa ni pamoja na: dhamira za kisiasa, ujenzi wa jamii mpya, mapenzi, utawala, nafasi ya mwanamke na majigambo. Utafiti huu ulibaini kuwa dhamira hutofautiana kati ya sitiari za majina ya Marais na sitiari za majina ya wasanii wa Muziki wa Bongo Fleva. Zipo dhamira ambazo zimejitokeza katika makundi yote na zipo ambazo hazijajitokeza katika makundi yote. Hii ni kwa sababu makundi haya ni makundi yenye dhima na nafasi tofauti katika jami**.**

**Hitimisho**

Makala hii imejadili kuhusu mchomozo wa usitiari katika majina ya viongozi na watu maarufu. Makala haya yalibaini kila jina huwa na maana na hutolewa kwa kuzingatia sifa, tabia, uongozi na wakati maalumu ambao kiongozi huyo anaongoza. Sifa za uongozi, tabia ya uongozi na utekelezaji wa majukumu, uimara, ustadi na umahiri katika uongozi na utekelezaji wa majukumu kulingana na wakati, muktadha na matarajio ya jamii kwa kiongozi husika. Aidha, makala hii imejadili kuwa majina ya viongozi yanatumika kisitiari kuibua dhamira za uongozi bora, nafasi ya mwanamke, ujenzi wa jamii mpya, ujenzi wa uchumi, vita dhidi ya rushwa na ufisadi, ushajuaa na ushupavu, ukombozi wa fikra dhidi ya ukoloni mamboleo na matarajio ya jamii katika maendeleo ya kiuchumi, kisiasa na kijamii. Aidha, makala hii imejadili kuwa sitiari zinazotumika kwa watu maarufu hususan wanamuziki huwa ni tofauti na majina ya kisitiari ambayo viongozi wa kisiasa hupewa na wananchi. Msanii hujipa jina likiwa ni ishara ya majigambo na sifa kwa ajili ya uwezo wa kazi yake ya usanii.

Majina haya huwa yamebeba dhamira ya kibishara na majigambo na pia sifa juu ya umaarufu, nguvu, uwezo na ujasiri alionao msanii katika kazi yake ya sanaa. Mfano matumizi ya neno simba, tembo, mnyama, chui na majina mengine yanaashiria ufalme na nguvu za msanii ndani ya jamii na katika sanaa yake. Kwa upande wa viongozi sitiari za majina yao huwa zimeambatana na nguvu za utawala, uchapa kazi na uhodari katika ujenzi wa jamii mpya.

**Marejeo**


Agyekum, K. (2006). The Socialinguistics of Akan Personal Names. International Journal of Humanities and Social Science, 15(2), 206–23.

Abdul, A. (2013). Maana na Sababu za Kiisimujamii Kwenye Majina ya Koo za Kiluguru. Tasnifu ya M.A Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (Haijachapishwa).

Ardrey, R. (1970) The social Contract, A Personal Inquiry into the Evolutionary Souces of Order and Disorder, New York, Atheneum.

Azael, R. (2013). Maana ya Majina ya Asili Katika Jamii ya Kiuru. Tasnifu ya M.A Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dae es Salaam. (Haijachapishwa).

Baitan, B. (2010). A Mopho- Semantic Analysis of Ruhaya Person Names. (Unpublished) M.A Dessertation. University of Dar es Salaam

Beidelman, T. O. (1974). *Kaguru Names and Naming*, katika Journal of Anthropological Research, 30:281-93. The University of Chicago Press.

Buberwa, A. (2010). *Investigating Socialinguistic Aspects of Place Names. The case of Ruhaya in North-western Tanzania*. Tasnifu ya Umahiri (haijachapishwa), Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Chandler, D. (2002) *Semiotics for Beginners.* Aberystwyth: Aberystwyth University.

Chiumbo.A (2016) *Maana za majina ya watu katika jamii ya Wayao*. Tasinifu ya Uzamili ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Chulk, O. (1992). *Names from African: Their Origin, Meaning and Pronounciation*. Chicaco: John Benjamin Publishing.

Daiches, D. (1981). Desturi na Mila Zetu. Arusha: East Africa Publication Limited.

Dawling, T, (2004). "*Uquidisizwe" The Finisher of Nation, Naming and taking about HIV/AIDS and African Langueges,* (Unpublished paper) http:/www.African voice. co. Za/reseach. htm.

Denice, S. (2011). *Haja ya Kuundwa Kamusi ya Majina ya Watu ya Asili katika Jamii ya Wahaya*, Tasnifu ya shahada ya uzamili (haijachapishwa), Chuo kikuu cha Dar-es-Salaam.

Funk, E. R. (1997). *The Power of Naming*, imepakuliwa tarehe 21/11/2022 Katika http://www.feminista.com/archives/v1n4/malefem.html.

Guma, M. (2001). *The Cultural Meaning of Names Among Basotho of Southern Africa*. Nordic Journal of Africa Studies 10(3): 265 – 279.

Habwe, J. na Karanja, P. (2004), *Misingi ya Sarufi ya Kiswahili,* Nairobi: Phoenix Publishers.

Haji M.M. (2014). *Uchunguzi wa kiisimu wa mifumo ya utoaji majina ya mitaa katika mkoa wa Kusini Unguja*: (Haijachapishwa) Chuo kikuu cha Uganda, Kampala, Uganda.

James, D. (2011). *Ishara katika Kaptula la Max na Kijiba cha Moyo*, Tasnifu ya M. Kiswahili, Chuo Kikuu cha Nairobi, Kenya.

Jonas, L. (2013). *Maana na Misingi ya Uteuzi wa Majina ya Watu katika Lugha ya Kiha*. Tasnifu ya M.A Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (Hajachapishwa).

Katakami, H. (1997). *Personal Names and Modes of Address Among the Mbeere*, katika African Study Monographs,18(3,4):203-212.

Kofi, A (2006). "*The Socialinguistic of Akan Personal Names*" . Nordric Journal of African Studies, 15 (2): pp 206-235.

Manyasa, J. (2009), *Investigating the Basis of Naming People in Kisukuma*, M.A. (Linguistics) Dissertation, University of Dares-salaam.

Mapunda, G. (2014). *What Do my Students Call Me? Nicknaming of Lecturers by Students at University of Dar es Salaam.* Journal of Linguistics and Language in Education 8(1)90- 107.

Massamba, D. P. B. (2009), *Kamusi ya Isimu na Falsafa ya Lugha*, chapa ya pili, Dar-es-Salaam: TUKI.

Mbiti, J. S. (1991) *Introduction to African Religion*, second edition, Nairobi: East African Educational Publishers Ltd.

Mdee, J. S. (2010) *Nadharia na Historia ya Leksikografia,* chapa ya tatu, Dar-es-salaam: TUKI

Mdee, J. S., Njogu, K. na Shafi, A (2013) *Kamusi ya Karne ya 21,* toleo la pili, Nairobi: Longhorn.

Msanjila, Y. P, Kihore, Y. M na Massamba, D. P. B. (2009) *Isimu Jamii Sekondari na Vyuo*, Dar es Salaam:

Mulokozi, M. M. (1996) *Fasihi ya Kiswahili*, Dar es Salaam: Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Musyimi, D. M. (2011), *Maana za Majina ya Watu katika Jamii ya Wakamba*, Tasnifu ya shahada ya uzamili, Kenyatta University.

Mutembei, A.K (2009) *UKIMWI katika fasihi ya Kiswahili*, Taasisi ya Taaluma za Kiswahili chuo kikuu Dar Es Salaam.

Muzale, H. R. T. (1998). The Linguistic and Social – Cultural Aspects in Interacustrine Bantu Names. Kiswahili (61):28-49.

Nagy, J. (2010). Social Research Methods. New York: Allyn and Bacon,

Ngunga, A. S. A. (1997), *Class 5 Allomorphy in Ciyao*, University of Califonia.

Olenyo, M. M. J. (2011) "*What is in a Name? An Analysis of the Semantics of Lulogooli Personal Names"* katika International Journal of Humanities and Social science, Vol. I, no.20.

Omary, C. K. (1970). Person Names in Social- Culture Context. Journal of the Institutes of Swahili Research. Vol 2:40 Sept, 1970, University of Dar es Salaam.

Ota, O. (2002). *Edo Person Names and World View*, New Perspective in Edoid Studies; Nigeria.

Resani, M. (2014) *Semantiki na Pragmatiki ya Kiswahili*, Dar: Karljamer Print Technology.

Rubanza, Y. I. (2000). The Linguistic Creativity of Haya Personal Names. Journal of Institute of Kiswahili Research, Vol. 63, TUKI, Dar es Salaam

Scholes, R. (1982) *Semiotics and Interpretation*, New Haven: Yale University Press.

Schotsman, P. (2003). Place Names and History in Dar es Salaam, Nadherland:Leiden University.

Seif, D. G. (2011). Nyimbo za Jando katika Jamii ya Kikaguru, Kata ya Gairo.Tasnifu M. A. Kiswahili, Chuo Kikuu Cha Dar-es-Salaam.

Sitati, V. W. (2007) *Comprehensive Names Dictionary*. Nairobi: Sas Enterprise.

TATAKI (2013) *Kamusi ya Kiswahili Sanifu,* Toleo la tatu, Dar: Oxford University Press.

TUKI (1990) *Kamusi Sanifu ya Isimu na Lugha,* Dar-es-Salaam: TUKI.

TUKI, (2004). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*; TUKI: Dar –es- Salaam.

Wacharo, (2013). Nyimbo za Jando katika Jamii ya Kikaguru, Kata ya Gairo.Tasnifu M. A. Kiswahili, Chuo Kikuu Cha Dar-es-Salaam.

Wafula, K. W., na Njogu, K. (2010). Nadharia za Uhakiki wa Fasihi. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Wamitila, K. W. (2002). Uhakiki wa Fasihi: Misingi na Vipengele Vyake. Nairobi: Phoenix Publishers

Whiteley, W. H. (1966), A *Study of Yao Sentences*, Oxford: Oxford University.

World Book Encyclopedia (1987), *N-O,"Name"*, Volume 14, Chicago: World Book, Inc.

https://radiojambo.co.ke/burudani/dakia-udaku/2022-07-19-diamond-afichua-asili-ya-jina-lake-la-utani-chibu-dangote/

https://www.udakuspecially.com/2016/11/diamond-aelezea-sababu-ya-kujiita-jina.html)